 - a) Kitaifa- kutakuwa na Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa wa World Revival Church na World Revival Ministries, Tanzania Inc ambaye atakuwa Mwenyekiti wa vikao vyote vya Kamati ya Utendaji, Mwenyekiti wa Wadhamini, na Baraza Kuu la World Revival Church(WRC).
 - b) Mkoa- kutakuwa na askofu wa Mkoa ambaye atakuwa mwenyekiti katika vikao vyote vya mkoa vya World Revival Church(WRC) ambaye atasimamia Makanisa yote ndani ya Mkoa na askofu wa mkoa atateuliwa na Askofu Mkuu.
 - c) Wilaya- kutakuwa na askofu wa wilaya ambaye atakuwa mwenyekiti katika vikao vyote vya wilaya vya World Revival Church(WRC) ambaye atasimamia Makanisa yote ndani ya wilaya na askofu wawilaya atateuliwa na Askofu Mkuu.
 - d) Kanisa la Mahali –kutakuwa na Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la mahali ambaye ataidhinishwa na Askofu Mkuu wa World Revival Church(WRC) na Mchungaji Kiongozi atashirikiana na Wazee wa Kanisa kwa kufuata Katiba(2002) na Kanuni(2009) za World Revival Ministries, Tanzania.
- iii. World Revival Church taifa au Ofisi Kuu litaongozwa na Kamati ya Utendaji Taifa ambao ni Mwenyekiti Mtendaji Taifa(Askofu Mkuu), Makamu Mwenyekiti Taifa(Askofu Mkuu Msaidizi), Katibu Mkuu Taifa (Askofu Mkuu Msaidizi, Mhasibu Taifa (Askofu Mkuu Msaidizi) ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Utendaji wa World Revival Ministries, Tanzania (W.R.M.T) kulingana na nafasi zao na majukumu yao kwa kufuata Katiba(2002) na Kanuni(2009 na Sheria na Maelekezo ya Utumishi(2002) ya World Revival Ministries, Tanzania (W.R.M.T).Wajumbe hao watachaguliwa kila baada ya miaka mitano (5) kwa miaka kumi(10) isipokuwa Mwenyekiti Mtendaji Taifa(Askofu Mkuu) ambaye anateuliwa kwa kufuata Katiba ya World Revival Ministries, Tanzania (W.R.M.T) ya mwaka 2002 na Wajumbe wengine wote ndani ya Kamati ya Utendaji hii wanachaguliwa kwa kutumia Kanuni za World Revival Ministries, Tanzania ya mwaka 2009 na kuchaguliwa kwao kwa kufuata Kanuni za World Revival Ministries, Tanzania ya mwaka 2009 watachukua majukumu yote yaliyoorodheshwa kwenye Katiba ya World

Revival Ministries, Tanzania ya mwaka 2002 bila kuchaguliwa tena na wote kwa pamoja watafuata utaratibu wa kazi ufuatao katika Kupanga, Kutekeleza, kusimamia, kutathimini, kujenga na kuimarisha World Revival Church (W.R.C.).

A. Mwenyekiti Mtendaji Taifa

- i. Atakuwa ndiye Msemaji Mkuu kwa niaba ya Kamati ya Utendaji, Maaskofu wa mikoa na wilaya, Wachungaji Viongozi wa makanisa ya mahali na pia Kanisa zima.
- ii. Ataongoza vikao vyote vya Kamati ya Utendaji na Baraza kuu la Kanisa.
- iii. Atakuwa ndiye Mwangalizi Mkuu wa World Revival Church au Askofu Mkuu kwa kufuata Kifungu cha 11(ii) cha Katiba ya World Revival Ministries, Tanzania(W.R.M.T) ya mwaka 2002.
- iv. Atasimamia Kamati ya Utendaji na shughuli zote za World Revival Church na World Revival Ministries, Tanzania hapa Tanzania.
- v. Atasimamia Neno la Mungu na Kanuni za World Revival Ministries, Tanzania-2009 katika kuendesha huduma hii.
- vi. Atawakilisha Kanisa kwenye mambo yote ya Kisheria.
- vii. Mwenyekiti atakuwa miongoni mwa waanzilishi wa World Revival Ministries, Tanzania (W.R.M.T) ili kusimamia maono haya hapa Tanzania.
- viii. Hataingilia makanisa ya mahali kiutendaji bali atasubiri mambo yote kutoka kwenye Baraza la Wazee ambayo yataletwa na Mchungaji Kiongozi wa kanisa la mahali husika kwa niaba ya Baraza la Wazee na ndipo Mwenyekiti Mtendaji Taifa atayashughulikia mambo yote baada ya kupata kibali hicho kwa kushirikiana na Kamati ya Utendaji ya huduma hii.
- ix. Atakuwa miongoni mwa watia sahihi kwenye mambo yote ya benki.
- x. Ataidhinisha Mchungaji wa World Revival Church kwenye eneo jipya kwa kufuata Kifungu cha 11(ii) cha Katiba ya World Revival Ministries, Tanzania ya mwaka 2002
- xi. Awe na sifa njema na mwenendo unaofaa kuigwa.
- xii. Awe amewahi kuwa Mtume, Mwinjilisti, Nabii, Mchungaji na Mwalimu ndani ya World Revival Ministries, Tanzania Inc na World Revival Church.
- xiii. Awe na sifa kama zinavyotajwa katika Tito 1:7-9.
- xiv. Asiyekumbatia uovu kwa maslahi yake binafsi
- xv. Awe na uwezo mkubwa wa kusimamia kazi yake katika misingi ya Kiroho
- xvi. Awe mume wa mke mmoja.
- xvii. Ataliwakilisha kanisa katika mialiko, sherehe, na mikutano mbalimbali ya Kiroho na serikali ndani na nje ya Tanzania.
- xviii. Kwa kushirikiana na Kamati ya Utendaji taifa atahakikisha usalama wa kanisa kupitia kusimamia na kutoa miongozo kwa ngazi zote za uongozi kwa kuhakikisha nidhamu ndani ya kanisa inatekelezwa na waamini bila kukiukwa misingi ya Biblia, Kanuni na Katiba ya World Revival Ministries, Tanzania Inc.

- xix. Kulinda, kuheshimu na kusimamia uhuru wa kila kanisa la mahali.
- xx. Kupokea maono ya makanisa ya mahali nchini kwa kushirikiana na viongozi wengine.

B. Makamu Mwenyekiti Taifa.

- i. Atakuwa tayari kumsaidia Mwenyekiti Mtendaji Taifa wa World Revival Ministries, Tanzania kwa shughuli zote za Kihuduma atakazompaa katika Ofisi yao.
- ii. Atashirikiana kila hatua na Mwenyekiti Mtendaji Taifa/Askofu Mkuu kwa ajili ya kuendesha Huduma/Kanisa hii.
- iii. Kama Mwenyekiti Mtendaji Taifa/Askofu Mkuu hayupo basi Makamu Mwenyekiti Taifa atachukua majukumu yote anayofanya Mwenyekiti Mtendaji Taifa/Askofu Mkuu.
- iv. Kutoa ushauri kwa Askofu Mkuu kuhusu maendeleo ya Kanisa
- v. Sifa za Makamu Askofu zitakuwa kama zilivyoielezwa za Askofu Mkuu wa Kanisa.

C. Katibu Mkuu Taifa.

- i. Atafanya shughuli zote za Ukatibu ikiwa ni kuandika taarifa za kila kikao na kuandika muhtasari ya mambo yote.
- ii. Atatunza kumbukumbu za Ofisi.
- iii. Atatunza nyaraka za huduma hii
- iv. Atashirikiana na Kamati ya Utendaji ya World Revival Church(W.R.C.) na World Revival Ministries, Tanzania(W.R.M.T) kwa kila hatua.
- v. Awe mwenye elimu ya angalau Shahada ya kwanza katika fani ya uongozi, utawala, uchumi, sosholojia, maendeleo ya jamii, sheria au elimu yoyote ya shahada.
- vi. Awe mwenye umri usiopungua miaka 35.
- vii. Atakuwa Katibu wa Kamati ya Utendaji wa World Revival Church (W.R.C.) na World Revival Ministries, Tanzania(W.R.M.T)
- viii. Atakuwa Katibu wa Baraza kuu la World Revival Church.
- ix. Atapokea barua kutoka kwa Wachungaji viongozi kutoka makanisa ya mahali ya World Revival Church.
- x. Atakuwa miongoni mwa watia sahihi kwenye mambo yote ya Kibenki.
- xi. Katibu mkuu atakuwa mtendaji mkuu wa utekelezaji wa shughuli za kiutawala za World Revival Church.
- xii. Katibu mkuu atawajibika moja kwa moja kiutendaji kwa Askofu Mkuu wa kila tendo la Kanisa.
- xiii. Katibu Mkuu atakuwa atakuwa msimamizi mkuu wa utekelezaji wa mipango mbalimbali ya WORLD REVIVAL CHURCH na shughuli zote za WRC kwa ujumla ikiwapo na usimamiaji wa utekelezaji wa mpango mkakati wa WRC wa wakati husika.

D.Mhasibu Taifa

- i. Makanisa yote ya mahali ya World Revival Church yanajiamulia yenyewe matumizi ya fedha zake, zaidi ya hayo kutakuwa na mahitaji yasiyoweza kutimizwa na kanisa la

mahali wala hayalihusu kanisa moja, kwahiyo kutakuwa na fedha ya pamoja zitakazotokana na Sadaka, Michango na pia Misaada kwa ajili ya matumizi ya World Revival Church taifa, kwahiyo Mhasibu Taifa atatumiza fedha hizo kwa ajili ya matumizi ya Makanisa yote ya World Revival Church(W.R.C.) na atazitoa kulingana na uhitaji uliopo wa Kanisa kwa maelekezo ya Kamati ya Utendaji.

- ii. Ataweka fedha benki na kutoa risiti kwa kila anapotoa au kupokea fedha za Kanisa
- iii. Atatumiza nyaraka za fedha
- iv. Atatoa taarifa ya fedha kwenye Kamati ya Utendaji na pia Baraza kuu
- v. Atabuni vyanzo vingine vya mapato vya Kanisa kwa kushirikiana na Kamati ya Utendaji
- vi. Atakuwa miongoni mwa watia sahihi kwenye mambo yote ya Kibenki.

FUNGU LA SITA

Kazi ya Kamati ya Utendaji ya World Revival Church.

- i. Kujenga ushirikiano kati ya makanisa ya World Revival Church.
- ii. Wataongoza World Revival Church kwa kufuata msingi wa Neno la Mungu, Katiba(2002), Kanuni(2009), Sheria na Maelekezo ya Mtumishi(2002) ya World Revival Ministries, Tanzania(W.R.M.T).
- iii. Watachaguliwa na Wachungaji Wakuu waliowekewa mikono(Ordained Senior Pastors) wa makanisa ya World Revival Church hapa Tanzania kwa kufuata Kanuni za World Revival Ministries, Tanzania ya mwaka 2009, isipokuwa Mwenyekiti Mtendaji Taifa atakaye chaguliwa kwa kufuata Katiba ya World Revival Ministries, Tanzania ya mwaka 2002.
- iv. Kuwasiliana na Wachungaji viongozi wa makanisa ya mahali ya World Revival Church kwa ajili ya kujua maendeleo ya makanisa ya mahali.
- v. Kutia moyo, kushauri na kuelimisha washiriki katika wajibu wao kwa Yesu Kristo
- vi. Kusaidia makanisa kujitegemea na kutegemeana.
- vii. Kuhimiza makanisa kutimiza wajibu wao kwa kuhubiri Injili na kujenga makanisa Kiroho
- viii. Kutembelea makanisa ya mahali hapa Tanzania
- ix. Kuanda kamati ndogondogo za Kanisa zima kulingana na uhitaji wa Kanisa.
- x. Kamati ya Utendaji kuliwakilisha Kanisa kwenye mambo ya Kisheria kwa kushirikiana na Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la mahali ambapo tatizo lipo.
- xi. Kamati ya Utendaji itaweka mikakati ya kuleta maendeleo ya kijamii yanayolenga kimwili, kiroho, na kiakili kwenye makanisa yote ya mahali ya World Revival Church.
- xii. Kamati ya Utendaji ndicho chombo kitaidhinisha Mchungaji Kiongozi kutumika katika Kanisa la Mahali lolote baada ya Mwanzilishi wa huduma hiyo kukoma kutumika hapa Tanzania na pia kumtoa kazini kwa kupokea matatizo ya Mchungaji Kiongozi kutoka kwenye Baraza la Wazee la Kanisa la mahali la World Revival Church kwa kuangalia Katiba(2002), Kanuni(2009), Sheria na Maelekezo ya Utumishi(2002) ya World Revival Ministries, Tanzania (W.R.M.T) na pia Neno la Mungu na pamoja na ufuatiliaji wa kina

na kuchunguza kwa umakini na ukaribu suala hilo kabla ya kuchukua hatua yoyote ili haki itendeke kuanzia kwa Waumini wote, wazee wote, mashemasi wote, Mchungaji Kiongozi, Wachungaji wa Idara, na pia Baraza zima la Wazee ndani ya mwaka mmoja tu hapo ndipo Kamati ya Utendaji itachukua hatua dhidi ya Mchungaji Kiongozi kumtoa kazini au kutomutoa kazini kwa maslahi ya Kanisa zima na pia kazi ya Mungu isiharibike na taarifa ya maamuzi yatapelekwa kwenye BARAZA KUU la Kanisa kwa taarifa tu na pia kwenye Uongozi wa World Revival Ministries, Tanzania.

- xiii. Watasimamia fedha na mali zote za World Revival Church kwa niaba ya Kanisa zima na mhasibu atafuata utaratibu wa kifedha kuhakikisha fedha zinatuzwa vizuri katika Akaunti ya Kanisa hapa Tanzania.
- xiv. Kupanga matumizi ya fedha kwa ajili ya kanisa zima
- xv. Itapokea mapendekezo ya maamuzi yao kutoka kwenye mabaraza ya wazee kwenye makanisa ya mahali kikatiba kwa kuyakubali au kuyakata kulingana na maslahi ya Kanisa la Mungu au taifa kwa ujumla na Mungu wetu tunayemtumikia.

FUNGU LA SABA

A. Yawepo Mabaraza ya Wazee ndani ya World Revival Church.

- i. World Revival Church ni Ushirika wa waliomwamini Bwana Yesu Kristo kuwa Bwana na Mwokozi wao na kubatizwa, kila Kanisa lina Mchungaji Kiongozi au Senior Pastor, Wazee wa Kanisa, Wachungaji wa Idara na Mashemasi.
- ii. Mchungaji Kiongozi na Wazee wa Kanisa wanalisimamia na kuliongoza Kanisa ambao ndio wanaunda BARAZA LA WAZEE(Matendo ya Mitume 20:17-18, 1 Timotheo 3:1-5. Wazee wa Kanisa wawe watu bila lawama wanaochaguliwa na Kanisa.
- iii. Wazee wa Kanisa wanalazimika kuwa na Vipawa na Karama tofauti maana ndio Wadhamini wa World Revival Church kwenye Kanisa la Mahali hapa Tanzania.
- iv. Mchungaji Kiongozi au Senior Pastor ni yeyote aliyepewa maono na Bwana Yesu Kristo kuanzisha kazi mpya sehemu yoyote hapa Tanzania au aliyekabidhiwa jukumu la kuchunga na Kamati ya Utendaji ya World Revival Church na Wazee wa Kanisa watachaguliwa na Kanisa zima na majina yao yakiwa yameletwa na kutajwa na Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la Mahali kulingana na maendeleo ya huduma yake kwa Uongozi wa Roho Mtakatifu lakini hatakuwa na mamlaka ya kumtoa kazini mpaka BARAZA LA WAZEE wakubaliane kama Timu ya Kiroho kwa kufuata Kanuni hii na Neno la Mungu, Mchungaji Kiongozi ambaye ni mwenye maono kutoka kwa Mungu hataingiliwa na Mtu yeyote katika huduma zake zote bali asivunje Neno la Mungu, Katiba(2002) na Kanuni(2009) na Sheria na Maelekezo ya Mtumishi(2002) za World Revival Ministries, Tanzania. Kanisa la mahali la World Revival Church hapa Tanzania litaongozwa na Mchungaji Kiongozi ambaye atakuwa Msemaji Mkuu wa Kanisa na Washauri wake ni Wazee wa Kanisa ambao watakuwa ni Wachungaji wasaidizi kwa Mchungaji Kiongozi, mamlaka ya kuliongoza Kanisa yako chini ya Mchungaji Kiongozi

wa kanisa la mahali hapa Tanzania kama alivyopewa maono ya kufanya kazi hiyo kutoka kwa Mungu.

- v. World Revival Church linatoa nafasi kwa wanaume na wanawake katika kumtumikia Mungu katika Yesu Kristo lakini sharti lazima wawe wameitwa na Mungu na Karama na vipawa kutambuliwa na Kanisa.

B. Kazi ya Baraza la Wazee wa World Revival Church.

- i. Kupanga kazi ya kanisa lao
- ii. Kuangalia maisha ya waumini, kuwalea Kiroho na kuchukua hatua za misaada inayohitajika hata kimwili baada ya Mchungaji Kiongozi kuleta kwenye kikao ambaye ni Mwenyekiti wa Baraza la Wazee.
- iii. Kupanga na kuangalia matumizi ya fedha za Kanisa kama Baraza la Wazee la World Revival Church chini ya Mwenyekiti wa Baraza la Wazee ambaye atakuwa Mchungaji Kiongozi au Senior Pastor pia Katibu na Mtunza fedha wa Baraza la wazee watachaguliwa na Baraza hilo kwa kura nyingi na watakuwa wanachaguliwa kila baada ya miaka miwili tu na Baraza la Kanisa la Mahali la World Revival Church hapa Tanzania na pia taarifa itatangazwa kanisani na maombezi maalum yatafanywa na Mchungaji Kiongozi.
- iv. Kutatua matatizo yote ya kanisa kwa kufuata Katiba ya Kanisa na Neno la Mungu na matatizo hayo yakishindikana yatapelekwa kwenye Kamati ya Utendaji kwa usuluhisho na kutoa maamuzi ya mwisho na hatimaye kupeleka maamuzi ya Kamati ya Utendaji kwenye Baraza Kuu kwa taarifa.
- v. Mchungaji Kiongozi atateua Mashemasi na kuwawekea mikono ya Baraka kulingana na uhitaji wa Kanisa 1Timotheo 3:8-13, Matendo ya Mitume 6:1-6 na atawapa kazi za kufanya za kanisa na kuwapa majukumu ya kufanya ndani ya kanisa la mahali la World Revival Church.
- vi. Mchungaji Kiongozi atakuwa mwenyekiti wa vikao vyote vya Baraza la Wazee.
- vii. Wazee wote wanaweza kupewa kazi au majukumu na Mchungaji Kiongozi kwa ajili ya maendeleo ya Kanisa.
- viii. Mchungaji Kiongozi ataitisha kikao baada ya yeye kama Mchungaji Kiongozi na aliyelitwa na Yesu Kristo kwa kuchunga kundi lake kushindwa kutekeleza suala lolote ndipo aitishie kikao cha BARAZA LA WAZEE akiwa na Agenda za tukio na maelezo ya kutosha kutoka kwenye Ofisi ya Kichungaji na si vinginevyo. Baraza halitaitwa kama hakuna agenda maalum ili kumfanya Mchungaji achunge vizuri na atumie huduma aliyopewa na Bwana Yesu Kristo bila kuingiliwa na wazee wa Kanisa.
- ix. Baraza la wazee wa Kanisa wanaweza kuomba kikao kwa mwenyekiti wa baraza la wazee baada ya kupata malalamiko mabaya ya kuharibu kazi ya Yesu Kristo kutoka kwa Waumini wa kanisa la mahali kwa njia ya barua inayoonyesha madhaifu ya Mchungaji Kiongozi wao na mashahidi wasio chini ya kumi(10) juu ya suala hilo na pia Baraza la

Wazee hilo la kanisa linaweza kufanya hivyo tena kama wanaona jambo haliendi vizuri juu ya Mchungaji wao ili kazi ya Mungu isiharibike na waumini wote walishwe sawasawa na Neno la Mungu, Baraza hilo litatoa ushauri tu na si kumfukuza na kama hali hiyo itaendelea zaidi ya mara tatu basi Baraza la Wazee wanaweza kutoa mapendekezo yao kwenye Kamati ya Utendaji bila kizuizi chochote Kikanuni kwa ajili ya kulinda kazi ya Mungu isihalibike na kwa maslahi ya Kanisa zima la World Revival Church. Lakini ni onyo kwa Baraza la Wazee kutoa siri hiyo kwa waamini hao tena kwasababu liko kiutendaji katika Ofisi ya Baraza la Wazee ambao ni Wadhamini wa Kanisa la World Revival Ministries, Tanzania, lakini kama ni taarifa mbaya ya uzinzi, kuiba, rushwa, kuua, na matukio mengine ya uharifu basi Baraza la wazee wapeleke taarifa hiyo moja kwa moja kwenye Kamati ya Utendaji na isiwe na kikao cha usuluhishi kwa maslahi ya kanisa zima na taifa kwa ujumla.

- x. Baraza la wazee ndio wenye mamlaka ya kutenga mshiriki ambaye amevunja IMANI na Madhumuni katika Kanisa la World Revival Church baada ya Mchungaji Kiongozi kushindwa kumlea Kiroho kutoa suala hilo kiofisi kama agenda ya kikao cha Baraza la Wazee.
- xi. Baraza la wazee na Mchungaji Kiongozi wataendesha Kanisa la Mungu kwa kufuata Neno la Mungu na kutambua kuwa Yesu Kristo ndiye Kichwa cha Kanisa.
- xii. Mchungaji Kiongozi wa kanisa ndiye Msemaji Mkuu kwa niaba ya Kanisa la Mahali, Wazee wa Kanisa na Waumini wote.
- xiii. Mchungaji Kiongozi na Wazee wa Kanisa watakuwepo kazini kwa muda usiojulikana kama Mungu alivyowaita kufanya kazi yake.
- xiv. Kamati ya Utendaji ya Taifa ya World Revival Church haina mamlaka kikatiba ya kuingilia Baraza la Wazee bali Kamati ya Utendaji itasubiri mambo yote kutoka kwenye Baraza la Wazee. Kamati ya utendaji itashughulikia mapendekezo yote kutoka kwenye Baraza la Wazee kama chombo kinachounganisha Mabaraza ya Wazee ya Makanisa ya mahali ya World Revival Church.
- xv. Mchungaji Kiongozi atakuwa huru kupokea maono mapya kutoka kwa Bwana Yesu Kristo lakini asivunje Neno la Mungu na Katiba(2002), Kanuni(2009) na Maelekezo na Sheria za Utumishi(2002) za World Revival Ministries, Tanzania na pia Baraza la Wazee lisimwingilie bali wamuombe na kumsaidia katika maono hayo.
- xvi. Mchungaji au mtu yeyote nje ya kanisa letu anaweza kuomba ushirika wa huduma aliyonayo kwa Mchungaji Kiongozi wa World Revival Church lakini akubaliane na Katiba(2002), Kanuni(2009) na Maelekezo na Sheria za Utumishi(2002) za World Revival Ministries, Tanzania kwa maandishi na asiwe mtu ambaye hana ushuhuda mwema kwenye huduma yake na atakuwa chini ya Uangalizi wa Mchungaji Kiongozi wa huduma hii na taarifa ipelekwe kwa Mwenyekiti Mtendaji Taifa.
- xvii. Mchungaji Kiongozi ataangalia shughuli zote za kanisa la mahali na kulinda kazi hiyo ya Mungu na pia kuanzisha kazi mpya katika maeneo mengine ili watu wengine wafikiwe na Injili ya Yesu Kristo na pia ataweka utaratibu wa makanisa hayo.

- xviii. Mchungaji Kiongozi aliyetwa na Yesu Kristo kuanzisha huduma au kazi yoyote chini ya World Revival Church atasaidiwa na kanisa hili maono yake aliyopewa na Mungu yafanyike bila kuingiliwa na mtu yeyote bali atafuata Katiba(2002), Kanuni(2009) na Maelekezo na Sheria za Utumishi(2002) za World Revival Ministries, Tanzania(W.R.M.T).
- xix. Mtumishi yeyote ataweza kuhubiri au kutoa Neno la Mungu lolote mbele ya Waumini kwenye ibada yoyote au mkusanyiko wowote baada ya kupata au kupewa na Mchungaji Kiongozi na si vinginevyo hii ni kumpa Mchungaji Kiongozi haki yake ya kuchunga Kanisa la Mungu maana yeye ndiye atakaye ulizwa mbele za Mungu.
- xx. Kikao cha Baraza la Wazee cha World Revival Church kitaitishwa na Mchungaji Kiongozi ambaye atakuwa Mwenyekiti wa kikao hicho pale anapoona kuna uhitaji wa kufanya hivyo.
- xxi. Mchungaji Kiongozi atakuwa na mamlaka ya Kichungaji ya kupanga ratiba ya ndani na nje ya Kanisa kwenye huduma yoyote au anaweza kuwapa Wazee wa Kanisa kumsaidia kama hayupo.
- xxii. Ni kazi ya Mchungaji Kiongozi , Wazee wa kanisa, Wachungaji wa Idara mbalimbali kutunza Siri za kanisa na pia kusaidia Waamini pale wanapoona badiliko lolote kwa ajili ya Kujenga mwili wa Yesu Kristo na si kuubomoa.

FUNGU LA NANE

A. Ziwepo Kamati za Idara ndani ya World Revival Church.

Idara za Kanisa za World Revival Church(W.R.C.) hizi zifuatazo na zitaongozwa na Mchungaji wa idara husika mwenye Kipawa na huduma ndani yake tu na watawekewa mikono na Mchungaji Kiongozi wa kanisa la mahali wa World Revival Church hapa nchini Tanzania na kama mtu hana kipawa hicho husika asiwekewe mikono kabisa.

- i. Idara ya watoto itaongozwa na Mchungaji wa Watoto.
- ii. Idara ya vijana itaongozwa na Mchungaji wa Vijana
- iii. Idara ya wanawake itaongozwa na Mchungaji wa Wanawake
- iv. Idara ya chuo cha biblia itaongozwa na Mkuu wa Chuo
- v. Idara ya shule ya msingi, sekondari, vyuo vya ufundi, chuo kikuu itaongozwa na Wakuu wa Shule na Vyuo.
- vi. Idara ya uinjilisti na umisheni itaongozwa na Mchungaji wa uinjilisti na umisheni
- vii. Idara ya uimbaji itaongozwa na Mchungaji wa uimbaji
- viii. Idara ya maombi itaongozwa na Mchungaji wa maombi na maombezi
- ix. Idara ya wanaume itaongozwa na Mchungaji wa wanaume
- x. Idara ya familia itaongozwa na Mchungaji wa familia.

B. Idara za World Revival Church zitafuata utaratibu ufuatao katika kujenga mwili wa Yesu Kristo.

- i. Kila idara inatoa ripoti ya kazi yake mara moja kwa mwaka kwenye kikao cha Baraza kuu kupitia Mchungaji Kiongozi wa kanisa la mahali.
- ii. Mchungaji Kiongozi wa kanisa la mahali ndiye Mlezi Mkuu wa idara zote kwenye Kanisa la mahali la World Revival Church hapa Tanzania.
- iii. Wachungaji wa idara watapokea ushauri wa kiidara kutoka kwa Mchungaji Kiongozi wa kanisa la mahali.
- iv. Kila Mchungaji wa idara ndiye atakuwa Msemaji Mkuu wa idara na atawajibika kiutendaji kwa Mchungaji Kiongozi.
- v. Mchungaji wa idara atatolewa kazini pale anapovunja Katiba na Neno la Mungu na Mchungaji Kiongozi kwa maslahi ya mapana ya kazi ya Mungu.
- vi. Wachungaji wa idara wataonyesha upendo, umoja, imani, kwenye idara zao ili kazi ya Yesu Kristo ijengwe.
- vii. Wachungaji wa idara hawatakuwa na mamlaka ya kutenga / kufukuza washiriki kwenye idara zao bali malalamiko yao yote yatapelekwa kwa Mchungaji Kiongozi wa kanisa la mahali ambaye ni Mlezi Mkuu wa idara zote.
- viii. Idara hazitakuwa na mamlaka ya kukusanya sadaka yoyote bali kazi hiyo itakuwa ya Baraza la Wazee ambao ni Wadhamini wa Kanisa la World Revival Church kwa kuweka utaratibu unaofaa kulingana na mahitaji ya Kanisa.
- ix. Mhubiri yeyote ndani ya idara yoyote ya World Revival Church lazima aidhinishwe na Mchungaji wa Idara kwanza na baadaye Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la mahali.
- x. Mhubiri yeyote wa idara anaweza kuwa ni Mwinjilisti, Mwalimu, Mchungaji, Mtume, Nabii, Mwimbaji, Mwombaji na si vinginevyo na wawe wametoka kwenye makanisa ya Kipentekoste tu.
- xi. Kila idara itajitegemea kiutendaji na kiuongozi ambapo Mchungaji wa idara atachagua wajumbe wa kamati ya idara yake wasiozidi wane(4) wenye karama na huduma hiyo ili wamsaidie kuwasha moto wa Injili ya Yesu Kristo kwenye idara husika na ana mamlaka ya kikatiba kumwachisha mjumbe anapoenda kinyume na utaratibu wa idara lakini mpaka Mchungaji Kiongozi akubali ombi lake, katika wajumbe wane(4) wawili watachaguliwa kuwa Katibu na mtunza fedha za idara watakaoendesha idara pamoja na Mchungaji wa idara ambaye ni Mwenyekiti wa Idara ndani ya World Revival Church kwenye Kanisa la mahali.
- xii. Kila idara ya Kanisa la World Revival Church itasaidiana na idara nyingine kwa mapatano kati ya Mchungaji wa idara husika kwa ajili ya kujenga mwili wa Yesu Kristo.
- xiii. Idara yoyote itapanua maono yake bila kuingiliwa na mtu yeyote lakini wasivunje Katiba na Neno la Mungu kwa ajili ya kujenga mwili wa Yesu Kristo.
- xiv. Ofisi ya Mchungaji Kiongozi ndiyo itakuwa kiunganishi kati ya Idara na Baraza la Wazee kiutendaji na si baraza la wazee kuingilia Idara kiutendaji.

FUNGU LA TISA

Yawepo Mabaraza ya Maaskofu ya Mkoa na Wilaya ndani ya World Revival Church.

Kwa kufuata Kifungu cha 17(e) cha Katiba ya WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA(W.R.M.T) ya mwaka 2002, Kamati ya Utendaji ya Kitaifa itasimamia Maaskofu wa mkoa na wilaya kupitia Mwenyekiti Mtendaji Taifa na Askofu Mkuu, na Maaskofu wa mkoa na wilaya watafanya majukumu yafuatayo:-

- i. Kazi zote ambazo zimeelekezwa kwenye Kifungu cha 17(e) cha Katiba ya World Revival Ministries, Tanzania(W.R.M.T) ya mwaka 2002.
- ii. Maaskofu wa mkoa na wilaya watapeleleza kazi na Askofu Mkuu kwa kufuata Katiba(2002), Kanuni(2009) na Maelekezo na sheria za Utumishi (2002) za World Revival Ministries, Tanzania(W.R.M.T).
- iii. Maaskofu wa mkoa na wilaya watakuwa wasaidizi kwa Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa katika kupanga, kusimamia, kutekeleza, kutathimini shughuli zote za kiutendaji ndani ya World Revival Ministries, Tanzania(W.R.M.T) na World Revival Church(W.R.C.) kwenye mikoa na wilaya.
- iv. Maaskofu wa mkoa na wilaya watakuwa ni wenyeviti wa vikao vyote kwenye mkoa au wilaya kwa makanisa yote ya WORLD REVIVAL CHURCH na washiriki wa kikao hicho watakuwa Wachungaji Viongozi na Makatibu wa makanisa ya mahali wa World Revival Church ili kuendeleza shughuli za Yesu Kristo ndani ya Wilaya au Mkoa mara moja kwa miaka mine(4).
- v. Maaskofu wa mkoa na wilaya watakuwa karibu sana na Wachungaji Viongozi wa World Revival Church kwenye makanisa yote ya mahali kwenye wilaya na mikoa yao kwa kufuata Katiba(2002), Kanuni(2009) na Maelekezo na Sheria ya Utumishi(2002) za World Revival Ministries, Tanzania(W.R.M.T).

FUNGU LA KUMI

Liwepo Baraza Kuu la World Revival Church.

a). Wajumbe wake wawe hawa wafuatao

- i. Wajumbe wote wa Kamati ya Utendaji Taifa
- ii. Maaskofu wa mkoa na wilaya
- iii. Wachungaji Viongozi, Makatibu wa makanisa, Mitume, Wainjilisti, Manabii na Walimu wa Neno la Mungu kutoka Makaniasa ya mahali ya World Revival Church(W.R.C.).

b). Angalau mara moja kwa miaka mitano(5), wajumbe wote wakutane mahali pamoja kujadili mambo ya Kanisa zima na vikao hivyo vitaendeshwa na Mwenyekiti Mtendaji na Askofu Mkuu wa World Revival Ministries, Tanzania(W.R.M.T) na World Revival Church(W.R.C.) ambaye ndiye Mtendaji mkuu wa shughuli zote za huduma hii.

c). Kazi ya Baraza Kuu

- i. Kufanya marekebisho ya Kanuni za World Revival Ministries, Tanzania kwa niaba ya Waumini wote baada ya kushirikisha makundi yote husika.
- ii. Kushauri Kamati ya Utendaji Taifa juu ya Utendaji wao
- iii. Kuchagua Kamati ya Utendaji Taifa kwa kufuata miongozo ya huduma.
- iv. Kujadili mambo yanayohusu Kanisa zima kwa ujumla kwa ajili ya maendeleo ya Kanisa na jamii.
- v. Kupeana mbinu bora mbalimbali za Kihuduma
- vi. Kushauriana na kuonyana kwa kufuata Neno la Mungu
- vii. Kujenga ushirikiano wa kanisa zima
- viii. Kusaidiana na kutia moyo Wachungaji Viongozi na Makatibu wao.

FUNGU LA KUMI NA MOJA

Kutengeneza Kanuni za World Revival Ministries, Tanzania za mwaka 2009.

Kanuni hizi zinaweza kutengenezwa kama neno au maneno yakipatikana ya kuongeza au kupunguza au kurekebisha mabadiliko hayo yanatayarishwa na Kamati ya Utendaji Taifa na kuyaomba kabla hawajapiga kura, ni sharti theluthi mbili za kura zote zipatikane ili matengenezo hayo yakubaliwe na hayo yote yatafanyika baada ya kuidhinishwa na makundi yafuatayo kwa asilimia 60 ya kila kikundi na kama kikundi chochote kitakata basi mabadiliko yoyote hayatafanyika kwa maslahi mapana ya Kanisa hili la World Revival Church na pia World Revival Ministries, Tanzania hapa Tanzania.

- i. Mabaraza ya wazee ya World Revival Church.
- ii. Wadhamini wa World Revival Ministries, Tanzania (W.R.M.T).
- iii. World Revival Ministries, Tanzania
- iv. Kamati ya Utendaji ya World Revival Church na World Revival Ministries, Tanzania
- v. Baraza Kuu la World Revival Church.
- vi. Mabaraza ya familia yote
- vii. Wanzilishi wa World Revival Ministries, Tanzania

FUNGU LA KUMI NA MBILI

Kuvunjwa kwa World Revival Church.

- i. World Revival Church(W.R.C.) halitavunjwa kwa uamuzi wa makusudi au uamuzi kwa kupiga kura wa waamini wa Kanisa. Kwa kuwa kanisa letu ni la Kiroho hatutarajii kuvunjika ila kanisa hili litaendelea kuhubiri Neno la Mungu hadi kurudi kwake Yesu Kristo

- ii. Muumini yeyote ambaye kwa sababu iwayo yote, anapoteza au kuiasi imani yake aondoke kwa utulivu na amani kutoka katika kusanyiko lolote la Kanisa la WORLD REVIVAL CHURCH na kuwaacha waumini waendeleo na kazi ya Bwana.
- iii. Kama Waanzilishi wa huduma hii watakubaliana kwa kura ya asilimia 60 na pia Wadhamini wa World Revival Ministries, Tanzania kama watakubaliana kwa kiwango hicho na baadaye kupelekwa kwenye Baraza Kuu la Kanisa na kupata zaidi ya asilimia 60 basi World Revival Church litavunjwa. Kama kusanyiko lolote la Kanisa la WORLD REVIVAL CHURCH linakuwa na migogoro au matatizo yanayopelekea kuvunjika kwa kusanyiko hilo, Kamati ya Utendaji chini ya Askofu Mkuu itasimamia kusanyiko hilo lisivunjike kwa kuchukua hatua zitakazofaa kulisaidia kusanyiko hilo.
- iv. Ingawa hatutarajii kanisa la WORLD REVIVAL CHURCH kuvunjika isipokuwa pakiwepo na sababu zozote za msingi zisizozuilika na zenye uthibitisho usio na mashaka kanisa linaweza kuvunjika ikitokea hali hii kanisa kulazimika kupiga kura.
 - a) Jina na mali zote za World Revival Church na World Revival Ministries, Tanzania zitachukuliwa na Kanisa/ Huduma lenye IMANI na MADHUMUNI sawasawa kwa kufuata sheria za Tanzania.
 - b) Hakuna fedha wala mali yoyote ya World Revival Church na World Revival Ministries, Tanzania itagawanywa kwa Waumini au Kiongozi yeyote wa Kanisa/Huduma kwa kufuata sheria za nchi.
 - c) Ni zaidi ya asilimia 70 ya wapiga kura wote wa kanisa ndio watakuwa na uwezo wa kuvunja Kanisa la World Revival Church kwenye kusanyiko lolote la mahali.
 - d) Mali zote ambazo ni sadaka, michango au misaada zitabaki chini ya uangalizi wa Bodi ya Udamini wa World Revival Ministries, Tanzania Inc.
 - e) Kama kutakuwa na madeni ya Kanisa hilo sehemu ya mali ya kanisa zitauzwa ili kulipia madeni hayo
 - f) Na kwa sababu kazi za WORLD REVIVAL CHURCH ni za kutangaza Injili ya Yesu Kristo duniani kote mali na fedha zitakazobakia baada ya migawanyo hapo juu(e) zitatolewa na kugawanywa kwa makanisa ya mahali mengine yenye malengo sawa na Kanisa la WORLD REVIVAL CHURCH ambayo yatazitimia mali na fedha hizo kiitangaza Injili ya Yesu Kristo.

FUNGU LA KUMI NA TATU.

Liwepo Baraza la Wadhamini la World Revival Church.

- i. Baraza la Wadhamini wa mali ya World Revival Church of Tanzania ambao ni wajumbe wa World Revival Ministries, Tanzania(W.R.M.T) kwa kufuata Sheria za Nchi liwe na wajumbe sio chini ya tisa(9) na wasiwe pungufu ya watatu(3) kwa kufuata Katiba ya World Revival Ministries, Tanzania (W.R.M.T) ya mwaka 2002 na usajili wake. Wadhamini hujulikana kwa jina la **“The Registered Trustees of the WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA (W.R.M.T)”**. Wadhamini wawe watu

- waaminifu wa Kiroho huchaguliwa kutoka kwa Waanzilishi, Kamati ya Utendaji na Wajumbe wa Baraza Kuu waliowekewa mikono/ Ordained Senior Pastors.
- ii. Kamati ya Utendaji kupitia Mwenyekiti Mtendaji na Askofu Mkuu inapendekeza majina kumi na tano(15) halafu Wachungaji waliowekewa mikono(Ordained Senior Pastors) linachagua majina tisa (9) kwa njia ya kupiga kura au kuteua au kuidhinisha, watu tisa(9) wenye kura nyingi watakuwa wadhamini. Wasipopatikana watu tisa(9) kwasababu ya usawa wa kura Ordained Senior Pastors watachagua upya kati ya wale wenye kura sawa. Mwenyekiti wa Kamati ya Utendaji Taifa wa World Revival Ministries, Tanzania ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya World Revival Ministries, Tanzania.
 - iii. Wadhamini watakuwa wajumbe kwa muda wa miaka sita (6), Mdamini anaweza kujiuzulu akitoa taarifa kwa maandishi kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Utendaji Taifa kwa kupitia kwa Baraza la Wadhamini.
 - iv. Kama mjumbe yeyote wa Kamati ya Udamini akiishi kinyume cha madhumuni na Imani ya World Revival Church ni juu ya Kamati ya Utendaji kupima mambo yake na kumwomba ajiuzulu au kumwondoa kazini.
 - v. Kama Mdamini akifa au kujiuzulu au kuondolewa kazini atachaguliwa mwingine badala yake kwenye kikao cha Baraza Kuu kifuatacho kwa pendekezo la KAMATI YA UTENDAJI TAIFA.
 - vi. Kila baraza la wadhamini linakuwa na Mwenyekiti na Katibu huchaguliwa kwa kufuata Katiba ya World Revival Ministries, Tanzania ya mwaka 2002 Kifungu cha Ishirini na mbili (22) hii ni pamoja na wajumbe wote wa Baraza la Wadhamini.
 - vii. Kazi ya Baraza la Wadhamini ni kutunza na kutawala viwanja vyote, nyumba zote, fedha zote na mali zote za World Revival Ministries, Tanzania na huduma zake kwa kufuata Katiba(2002), Kanuni(2009) na Maelekezo na Sheria za Utumishi(2002) za World Revival Ministries, Tanzania kwa niaba ya huduma na Kanisa.
 - viii. Baraza la Wadhamini hukaa kikao kwa mwaka mmoja, maazimio yote huamuliwa kwa njia ya wingi wa kura, na idadi ya wajumbe kwenye vikao isiwe chini ya tano(5) kama Wadhamini wote ni tisa (9).
 - ix. Katibu huandika muhtasari za kila kikao na nakala zake hupelekwa kwa wajumbe wa Baraza la Wadhamini na Kamati ya Utendaji na hatimaye Baraza Kuu.
 - x. Katika mambo yote ya kisheria Bodi ya Wadhamini ya World Revival Ministries, Tanzania (W.R.M.T) itashirikiana kwa ukaribu na Maaskofu wa mkoa na wilaya na pia Wachungaji Viongozi wa makanisa ya mahali ya World Revival Church(W.R.C.) kwa kufuata Katiba(2002), Kanuni(2009) na Maelekezo na Sheria za Utumishi (2002) za World Revival Ministries of Tanzania(W.R.M.T).
 - xi. Wadhamini wasiwe na fungu la rasimali ya Kanisa/Huduma wala madai yoyote ya mali ya Kanisa/ Huduma.
 - xii. Mhuri maalumu (Official Seal) wa Wadhamini ni **“The Registered Trustees of the World Revival Ministries, Tanzania (W.R.M.T)”**.

- xiii. Mambo yote ya makabidhiano ya mali, nyaraka zozote, hati zozote ndani ya Baraza la Wadhamini wa World Revival Ministries, Tanzania (W.R.M.T) zitafanyika kwa maandishi na nakala za makabidhiano zitapelekwa kwenye Kamati ya Utendaji ya World Revival Ministries, Tanzania na World Revival Church.

FUNGU LA KUMI NA NNE

Liwepo Baraza la Familia ndani ya World Revival Church.

- i. World Revival Church of Tanzania litaanzia huduma yake kwenye familia au kaya moja moja katika kuhudumia watu KIROHO, KIMWILI NA KIAKILI ambapo baba na mama au kaka au binti ndani ya kaya au familia watakuwa ni wajumbe wa kudumu au mwamini yeyote ndani ya familia kwa kuleta watu wengi kwa Yesu Kristo kwenye maeneo mwamini anakoishi na ni Mjumbe ndani ya World Revival Church katika kujenga mwili wa Yesu Kristo.
- ii. Mchungaji wa familia atawasiliana na Mchungaji Kiongozi wa World Revival Church katika kujenga mwili wa Yesu Kristo.
- iii. Mchungaji Kiongozi kwa kushirikiana na mwamini kwenye familia au kaya atatoa msaada wowote wa Kiroho, Kimwili na Kiakili kulingana na uhitaji wa familia hiyo na pale anapoitwa na Mchungaji wa familia.
- iv. Familia itakuwa na Ibada nyumbani na itamuomba Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la mahali, Wazee wa Kanisa, Mashemasi, Wachungaji wa Idara mbalimbali, na viongozi wengine wa kimkoa na kiwilaya na pia Kitaifa na pia familia itasaidia Mchungaji Kiongozi pale Roho Mtakatifu anapowagusa kufanya hivyo kwa ajili ya Yesu Kristo na kazi yake.
- v. Mchungaji wa familia atatumia Neno la Mungu kuongoza familia yake na pia wageni
- vi. Mchungaji wa familia atasaidiana na Mchungaji Kiongozi wa kanisa la mahali la World Revival Church katika kujenga mazingira mazuri ya elimu ya watoto wa familia kwa ajili ya manufaa ya familia, kanisa na taifa.
- vii. Mchungaji wa familia atawasiliana na Mchungaji Kiongozi wa World Revival Church juu ya ratiba ya kanisa zima katika kusanyiko la mahali ambapo familia mbalimbali zitakusanyika pamoja kumwabudu Mungu kwa Upendo.
- viii. Familia zaidi ya moja zinaweza kuanda Ibada kwa kushirikiana kwenye eneo moja au mtaa mmoja kwa kushirikiana kwa makubaliano ila taarifa ipelekwe kwa Mchungaji Kiongozi wa World Revival Church kwa kanisa la mahali na atatuma mtumishi atakaye mwakilisha.
- ix. Baba/ Mama/Kaka/Dada aliyekoka ni Msemaji wa familia kwenye World Revival Church of Tanzania kwa ajili ya kueneza Injili ya Yesu Kristo kwenye familia hiyo.
- x. Mchungaji wa familia atakuwa ni mhimili kwenye eneo lake na anaweza kukaribisha kanisa zima kupitia Mchungaji Kiongozi kwa ajili ya mkutano wa Injili katika eneo lake kama kueneza injili ya Yesu Kristo ya nyumba kwa nyumba.

- xi. Mchungaji Kiongozi wa World Revival Church katika kusanyiko la mahali hapa Tanzania atafanya kazi yake kwa kushirikiana na wachungaji wa familia kwenye maeneo yaliyoandaliwa na Kanisa ili mwili wa Yesu Kristo ujengwe.
- xii. Familia tano (5) na zaidi zilizopo pamoja katika eneo moja zitachagua mchungaji wao wa familia hizo na Mchungaji wa familia hizo atashirikiana kwa ukaribu na Mchungaji Kiongozi wa World Revival Church, Mchungaji wa familia hizo atapeleka taarifa zote kwa Mchungaji Kiongozi, sharti la mchungaji huyo wa familia awe na kipawa na karama za kichungaji ili kanisa la Yesu Kristo lisigawanyike bali Upendo, Umoja na Imani viendelezwe kwenye familia na atafanya kazi zote za KISHEMASI katika familia hizo.
- xiii. Familia ya World Revival Church zitapokea taarifa za kiutendaji wa Kanisa kutoka kwa Mchungaji Kiongozi kama Msemaji Mkuu wa Kanisa la mahali na si vinginevyo., taarifa ambazo hazitolewa na Mchungaji Kiongozi ni batili na si za World Revival Church (W.R.C.).
- xiv. Ni kazi ya Mchungaji wa familia kutunza heshima ya Kanisa la Mungu kwa kujenga na si kuubomoa ili Mwili wa Yesu Kristo ujengwe vizuri na pia Wachungaji wa familia watateuliwa kuwa Mashemasi wa World Revival Church.

FUNGU LA KUMI NA TANO

Sherehe ndani ya World Revival Church.

- i. Sherehe zote zinazoendeshwa na Makanisa ya Kipentekoste ulimwenguni kama KRISMASI, MWAKA MPYA, PASAKA na NDOA ya Mke na Mme zinatambuliwa na World Revival Church(W.R.C.) na World Revival Ministries, Tanzania (W.R.M.T).
- ii. Mafunuo yoyote ambayo hayaendani na Neno la Mungu hayakubaliki ndani ya World Revival Ministries, Tanzania (W.R.M.T) na World Revival Church(W.R.C.)

FUNGU LA KUMI NA SITA

A. Kamati ya Nidhamu na Maadili ya World Reviva Church(W.R.C.)

- i. Itakuwepo kamati ya nidhamu na maadili ya WORLD REVIVAL CHURCH kwa ajili ya kusikiliza migogoro itakayojitokeza ndani ya Kanisa la mahali.
- ii. Kamati hii itakuwa na mamlaka dhidi ya waamini wote wa WRC na idara/ taasisi zake.
- iii. Kamati hii itakuwa chini ya baraza kuu na kwamba itawajibika kwa baraza kuu.
- iv. Lalamiko ni lazima liwe kwa maandishi na ni lazima lipitishwe na kiongozi yeyote wa kanisa ambalo mlalamikaji au mlalamikiwa anaabudu.

B. Wajumbe wa Kamati ya Nidhamu na Maadili ya WRC

- i. Maaskofu wa Mikoa
- ii. Askofu Mkuu Msaidizi Taifa-Mwenyekiti wa kikao
- iii. Mhasibu Taifa

C. Kazi ya Kamati ya Nidhamu na Maadili ya WRC

- i. Hiki ni chombo maalumu cha kushughulikia na nidhamu na maadili ya watumishi wote wa WRC pamoja idara na taasisi zake zote
- ii. Kufanya uchunguzi juu uhalisia wa lalamiko /tuhuma ili kuupata ukweli
- iii. Kutoa pendekezo kwa kamati ya utendaji wa kanisa
- iv. Lalamiko lolote linalohusu mienendo ya wachungaji na watumishi itapaswa iwekwe kwenye maandishi yapelekwe kwa Katibu Mkuu ambaye naye atapeleka malalamiko hayo kwenye Kamati ya nidhamu na maadili ya WRC.

FUNGU LA KUMI NA SABA

Baraza la Usuluhishi wa Ndoa(BUN)

Liwepo baraza la usuluhishi wa ndoa za Waamini wa World Revival Church.

A. Wajumbe wa Baraza la Usuluhishi.

Wajumbe wake huteuliwa na Wazee wa Kanisa wa Kanisa la Mahali na kuidhinishwa na Askofu Mkuu wa World Revival Church.

B. Sifa za Wajumbe wa Baraza la Usuluhishi wa Ndoa.

- i. Awe Muumini wa World Revival Church.
- ii. Awe Mkristo mwenye ndoa halali ya kanisani.
- iii. Awe na ushuhuda mzuri.

C. Kazi za Baraza la Usuluhishi wa Ndoa.

- i. Kufungisha ndoa kulingana na kanuni za Kikristo/ Kiroho na kulingana na sheria ya nchi.
- ii. Kushughulikia masuala yote ya migogoro ya ndoa ikiwa mchungaji wa kanisa la mahali ameshindwa kulipatia ufumbuzi.
- iii. Migogoro iliyoshindikana itakabidhiwa kwa maandishi kutoka kwa mchungaji aliyekuwa anashughulikia (ngazi ya kanisa la mahali)kupeleka katika Baraza la Usuluhishi la Ndoa.
- iv. Pia kuwepo na utaratibu mzuri wa kupeana taarifa kutoka baraza hili la usuluhishi kwenda kanisa la mahali hasa pale ambapo migogoro hiyo imefanikiwa kutatuliwa ama la na sababu za mafanikio yake, na
- v. Lakini pia, hata kama migogoro hiyo imeshindikana kupatiwa ufumbuzi, basi kuwepo na mapendekezo (kwa mujibu wa Biblia) ya nini kingefaa kufuatwa na mchungaji wa Kanisa la Mahali pale ambapo wenye mgogoro huabudu.

FUNGU LA KUMI NA NANE

Hati ya Kisheria ya World Revival Ministries, Tanzania na World Revival Church hapa duniani.

World Revival Church imeundwa kutokana na Katiba ya World Revival Ministries, Tanzania Kifungu cha 18(b)iv, 7(1), 10(x), 11(2) na Kanuni hii itafunga kila Muumini na

Kiongozi yeyote ndani ya World Revival Church(WRC) na Kanuni hii imeundwa kwa kufuata Katiba ya WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA ya mwaka 2002 na kuwa:-

- i. World Revival Ministries, Tanzania Inc ni huduma ya Kitume na Uinjilisti ambayo inahusisha Watumishi wote wenye miito tu sawasawa na Waefeso 4:1-18 ambao ni Wachungaji, Mitume, Wainjilisti, Manabii, Walimu wa Neno, Waimbaji na Viongozi wengine wa Mkanisa ya Kiroho kutoka Mkanisa ya Kipentekoste hapa duniani na huduma itajilenga kwa kuleta watu wengi kwa Yesu Kristo ambaye ni BWANA na MWOKOZI wetu na itafungua Mkanisa ya KIROHO yatakayoitwa WORLD REVIVAL CHURCH sawasawa na Katiba ya WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA kifungu cha 18(b)iv, 7(1), 10(x) na 11(2).
- ii. Kila Mtumishi au Muumini yeyote atalinda WORLD REVIVAL CHURCH na WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA.
- iii. Watumishi wenye miito ndani ya World Revival Ministries, Tanzania Inc ndo wenye mamlaka ya kuongoza Mkanisa ya mahali ya WORLD REVIVAL CHURCH sawasawa na Waefeso 4:1-18 tu.
- iv. Katiba ya World Revival Ministries, Tanzania ya mwaka 2002 na Kanuni hii ya World Revival Ministries, Tanzania Inc ya mwaka 2009 zitaendelea kuongoza Waamini na Viongozi wote kwa shughuli zote za kila siku.

FUNGU LA KUMI NA TISA

A. Mabaraza ya Washiriki au Waamini wa World Revival Church.

- i. Yawepo mabaraza ya Waamini wa Mkanisa ya mahali ya World Revival Church.
- ii. Zipo kanuni za vikao

B. Wajumbe wa Baraza la Waamini wa World Revival Church.

Wajumbe wake ni hawa wafuatao:-

- i. Mchungaji wa kanisa la mahali la World Revival Church.
- ii. Wazee wa Kanisa wa Kanisa la mahali la World Revival Church.
- iii. Mashemasi wote wa kanisa la mahali
- iv. Wachungaji wasaidizi wote wa kanisa la mahali
- v. Wainjilisti wote wa kanisa la mahali
- vi. Mitume wote wa kanisa la mahali
- vii. Walimu wote wa kanisa la mahali
- viii. Manabii wote wa kanisa la mahali
- ix. Waimbaji wote wa kanisa la mahali
- x. Wakristo wote ambao ni hai ndani ya Kanisa la mahali(Wasiotengwa na Ushirika)

C. Utaratibu wa Baraza la waamini au Washiriki wa World Revival Church.

- i. Hiki ni chombo chenye mamlaka ya mwisho kabisa katika kanisa la mahali la World Revival Church.
- ii. Baraza la waamini au washiriki litaongozwa na Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la mahali la World Revival Church.
- iii. Mahudhurio yanayohalalisha kikao cha kawaida kwa maamuzi ya kawaida yawe zaidi ya nusu ya wajumbe wa baraza la waamini au washiriki.
- iv. Mahudhurio yanayohalalisha kikao maalum kwa ajili ya maamuzi maalumu yawe zaidi ya theluthi mbili ya wajumbe halali wa baraza la waamini au washiriki.
- v. Maamuzi magumu , nyeti, na yale yanayotaka uadilifu na umakini mkubwa ni lazima yafanywe katika kikao maalumu na kamwe siyo katika kikao cha kawaida.
- vi. Tafsiri ya kikao maalumu inanzia katika idadi ya wajumbe na kisha katika majukumu ya kikao. Wajumbe wanaohudhuria kikao isiwe chini ya theluthi mbili ya wajumbe wanaopaswa kuhudhuria kikao hicho. Na mfano wa maamuzi magumu ni kama yale yanayogusa utambulisho wa kanisa, kuhamisha makao makuu ya ofisi, yanayogusa imani na madhumuni ya kanisa, yanayogusa kutengua vifungu vya kanuni na katiba ya World Revival Ministries, Tanzania, yanayogusa matumizi ya rasilimali kubwa za kanisa, yanayogusa mikataba, chaguzi ndani ya kanisa na kadhalika.
- vii. Tafsiri ya kikao cha kawaida nayo inanzia katika idadi ya wajumbe na majukumu ya kikao. Wajumbe wanaohudhuria kikao hicho isiwe chini ya nusu ya wajumbe wanaopaswa kuhudhuria kikao. Mfano wa maamuzi ya kikao cha kawaida ni yale ambayo hata kikao kikiwa na watu wachache sana kinaweza kutolea maamuzi bila kuashiria hulka na harufu ya ubinafsi, hujuma, au dhamira / ila mbaya.
- viii. Chini ya nusu hakuna kikao halali kinachoweza kukaliwa.
- ix. Theluthi mbili ya wajumbe inabadilisha hadhi ya kikao na kukifanya kuwa maalumu na hapo mambo yale makubwa makubwa yanaweza kujadiliwa na kupitishwa.
- x. Baraza la waamini au washiriki wa kanisa la mahali la World Revival Church hukaa kwa muda watakojipangia wenyewe pale ambao kuna jambo linalohusu kanisa zima ili kuwa na utekelezaji wa kazi za kanisa.

D. Kazi za Baraza la Waamini au Washiriki wa World Revival Church.

Kazi za Baraza la Waamini au Washiriki wa World Revival Church:-

- i. Katika kikao cha waamini mambo ya kanisa yanayowahusu waamini au wakristo wote yanajadiliwa(mikutano ya injili, ujenzi wa kanisa na mengine yenye kuhitaji kanisa zima kushiriki ipasavyo).
- ii. Kuwachagua wazee wa kanisa kwa kupiga kura majina yatakayopendekezwa na Mchungaji Kiongozi wa kanisa la mahali la World Revival Church.
- iii. Kuwachagua mashemasi ambao majina yao yatayopendekezwa na Mchungaji kiongozi wa kanisa la mahali wa World Revival Church.(1 Timotheo 3;8-13, Matendo ya Mitume 6:1-6).

- iv. Ni juu wa Waamini au washiriki wote wa kanisa la mahali la World Revival Church wakiongozwa na uongozi wa kanisa kutunza na kulinda majengo na mali nyingine ya kanisa la mahali kwa niaba ya World Revival Church na World Revival Ministries, Tanzania.
- v. Kukata shauri mambo yote yanayoletwa na Baraza la Wazee wa Kanisa la mahali.
- vi. Kumthibitisha mhasibu wa kanisa ambaye atakuwa amechaguliwa na Baraza la Wazee.
- vii. Kupokea, kujadili na kutoa ushauri kwa taarifa mbalimbali za utendaji kanisani.
- viii. Kutoa maoni kwa wazee wa Kanisa ili yakifaa yaweze kufanyiwa kazi.
- ix. Baraza la Wazee wa Kanisa la Mahali litawajibika kiutendaji kwenye Baraza la Waamini au Washiriki kwa kila tendo katika uendeshaji wa Kanisa la Mahali.
- x. Muumini au Kiongozi wa WORLD REVIVAL CHURCH(W.R.C) atakuwa mstari wa mbele kukataa na kukemea Jina na Usajili wa World Revival Ministries, Tanzania na World Revival Church kutumika kama mwavuli kwa huduma nyingine maana kitendo hicho ni Kuvunja sheria ya Nchi ya Tanzania.
- xi. Muumini au Kiongozi wa World Revival Church akitoa ardhi yake au kiwanja chake au sadaka yake itahesabika ni sadaka kwa Mungu na haitarudishwa na Waamini/Viongozi na Kanisa kwa ujumla.

FUNGU LA ISHIRINI

A. Mwanasheria wa World Revival Church na World Revival Ministries, Tanzania .

- i. Kutakuwa na Mwanasheria wa WRC na WRMT mwenye sifa ya kuwa wakili ambaye anateuliwa na Askofu Mkuu na kuthibitishwa na Kamati ya Utendaji ya Kanisa.
- ii. Kutakuwa na wasaidizi wa Mwanasheria wa WRC na WRMT wasiozidi wawili(2) ambao wanapaswa kuwa ni mawakili wanaotambuliwa na chama cha wanasheria cha Tanganyika.
- iii. Kitengo hiki cha sheria kitakuwa chini ya usimamizi wa moja kwa moja wa Ofisi ya Askofu Mkuu wa WRC na WRMT.

B. Kazi za kitengo cha sheria

- i. Kulinda haki za WRC na WRMT katika mashauri ambayo WRC na WRMT zinahusika.
- ii. Kuliwakilisha kanisa kwenye mambo ya kisheria.
- iii. Kushiriki katika majadiliano yoyote ya kisheria ambayo WRC na WRMT zinaenda kuwa washirika.
- iv. Kushauri Uongozi wa WRC na WRMT kwa mambo yote yanayohusu sheria.
- v. Kuanda nyaraka za kisheria pale inapobidi.

FUNGU LA ISHIRINI NA MOJA

Sadaka na Mgawanyo wake ndani ya World Revival Church(W.R.C) na World Revival Ministries, Tanzania (W.R.M.T).

- (i) Kwa kuwa Sadaka ni sehemu ya Ibada sawasawa na Neno la Mungu, kila Muumini na Kiongozi yeyote atambue kuwa Sadaka ni **IMANI** na ina matokeo makubwa **KIROHO** na **KIMWILI** na pia ina matokeo makubwa kwa anayetoa Sadaka aangalie anachokitoa kuwa kina mpendeza Mungu aliyemuumba kwa kumtolea Ibada inayompendeza Mungu sawasawa na Waebrania 12:28-29. Kwa kutambua Neno la Mungu **WORLD REVIVAL CHURCH** na **WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA** katika kutekeleza majukumu yake ya **IMANI** kila siku itagawanya Sadaka hiyo kwa matumizi ya Kanisa la Mahali na pia Ofisi Kuu kwa kufuata Mwongozo wa Kanisa kama ifuatavyo:-
 - a) **Asilimia kumi(10) au 10% itaendesha Ofisi Kuu.**
 - b) **Asilimia tisini (90) au 90% itaendesha Kanisa la Mahali husika.**
- (ii) Migawanyiko hii itawezesha shughuli za Ofisi kuu kama kusafirisha Watumishi wa Mungu ndani na nje ya Nchi katika kutekeleza majukumu yake ya Kanisa, kusaidia suala lolote la Ofisi kuu katika kutekeleza majukumu ya Kanisa, na kuanda mikutano ya pamoja ya Ofisi kuu katika kutekeleza shughuli za Kanisa. Migawanyiko hii pia itawezesha Kanisa la Mahali kubaki na kiasi kikubwa kuendesha shughuli mbalimbali za Kanisa na kumtunza Mchungaji ambaye ni Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la Mahali husika.
- (iii) Kwa kuwa Sadaka ni **IMANI** sawasawa na **NENO LA MUNGU** kila Muumini au Kiongozi ndani ya World Revival Church na World Revival Ministries, Tanzania Inc atasimamia kulingana na migawanyiko hiyo kwa ajili ya kujenga Ufalme wa Mungu katika Yesu Kristo.
- (iv) Kwa kusimamia Imani hii ya kujenga Ufalme wa Mungu sawasawa na Neno la Mungu. Kanisa hili litaendelelea kumtambua **Mchungaji Kiongozi** wa Kanisa la Mahali husika kwa kuwa **Mwaminifu** na **Mnyenyekevu** mbele za Mungu na Wanadamu katika kusimamia Imani hii na kuwa ni sehemu ya kujenga Ufalme wa Mungu na ambaye ni **Mtekelezaji Mkuu** wa shughuli zote za Kanisa la Mahali ndani ya World Revival Church na World Revival Ministries, Tanzania kwa kufuata Katiba(2002) na Kanuni(2009) za World Revival Ministries, Tanzania Inc(W.R.M. T).

©W.R.M.T/KANUNI - 2009.

MWONGOZO WA KANISA/HUDUMA UNAJUMUISHA NENO LA MUNGU(THE BIBLE), TENZI ZA ROHONI, KATIBA(2002), MAELEZO YA IMANI (2009), KANUNI(2009) NA MAELEKEZO YA KIBALI CHA MTUMISHI(2002).

WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA

(W.R.M.T)

“The Outreach Ministry for Gospel of Jesus Christ on the Earth”

P.O.BOX 6712 MOSHI-TANZANIA

Email: worldrevivalministries@yahoo.com

Phone: +255 786 19862, +255790198623, +255790198623



MAELEKEZO YA MTUMISHI-(2002)

©WRMT/MAELEKEZO YA MTUMISHI-2002

FUNGU LA KWANZA

Utangulizi

- i. World Revival Ministries, Tanzania yenye usajili **SA.17453** inatambua usimamizi wa Watumishi wake kwa kufuata Sheria za nchi, hata hivyo kifungu cha 11(2) cha Katiba ya World Revival Ministries, Tanzania ya mwaka 2002 inatoa mamlaka kwa Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa kuteua wasaidizi wake kwenye Ofisi yake katika kusimamia **KANISA LA MAHALI** ambao watawajibika wote kiutendaji kila siku kwa kila tendo la Kanisa kwenye Ofisi ya Askofu Mkuu katika kusimamia Waamini na Viongozi wote hapa nchini Tanzania.
- ii. Maelekezo ya Mtumishi ya mwaka **2002** imeundwa kwa kufuata kifungu cha **18(b)iv** cha Katiba ya World Revival Ministries, Tanzania ya mwaka 2002 katika kuongoza Waamini wote na Viongozi wote ndani ya World Revival Ministries, Tanzania na World Revival Church hapa Nchini Tanzania.
- iii. Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa atateua Mchungaji, Mtume, Mwinjilisti, Mwalimu wa Neno, Nabii na Mtumishi yeyote kutumika ndani ya **WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA** kwa kufuata Kifungu cha 11(2) cha Katiba ya **WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA** ya mwaka 2002.
- iv. Baada ya Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa kuteua Mtumishi husika basi Mtumishi huyo husika huyo atakuwa na mamlaka yaleyale kuteua timu ya Uongozi atakaofanya nayo kazi ambao ni Wachungaji Wasaidizi, Wazee wa Kanisa, Mashemasi na viongozi wengine katika kuongoza Waamini au Mikusanyiko ya Waamini au Kanisa la Mahali hata hivyo Sharti Kuu na la msingi wote ni kuidhinishwa na **BARAZA LA WAAMINI** au **WASHIRIKI** wa World Revival Church kwa kufuata Kanuni za World Revival Ministries, Tanzania ya mwaka 2009 Kifungu cha **Kumi na Tisa (19)**.
- v. World Revival Ministries, Tanzania itafungua au kuanzisha Makanisa ya Mahali yatakayoitwa **THE WORLD REVIVAL CHURCH** kwa ajili ya kukusanya Waamini kwa ajili ya **kusifu Mungu, Kuabudu Mungu, Kuomba Mungu, kufanya mahusiano na Mungu** kwa kufuata Kifungu cha 7(1), 10(x) na 11(2) cha Katiba ya World Revival Ministries, Tanzania ya mwaka 2002 na Makanisa ya Mahali yote yataongozwa na Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa na atateua Wachungaji Viongozi katika Ofisi yake kwa ajili ya kusimamia kila Kanisa la Mahali husika na **kila Mchungaji Kiongozi atawajibika Kiofisi kwa Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa. Kwa kila tendo katika Ofisi ya Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji.**
- vi. World Revival Ministries, Tanzania katika kufungua au kuanzisha kusanyiko lolote la Waamini , Mchungaji atahakikisha anafuata Maelekezo ya Imani ya mwaka 2009 ya World Revival Ministries, Tanzania namba 9 tu ili kulinda Waamini wote ndani ya Huduma/Kanisa.
- vii. World Revival Ministries, Tanzania inaelekeza kila Mchungaji mwenye kuongoza Waamini ndani ya World Revival Church of Tanzania kutoa **FUNGU LA KUMI (10%)**

kwa Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa wake kwa kufuata Kanuni (2009) ya World Revival Ministries, Tanzania kwa kufuata Kifungu cha **ishirini na moja (21)** katika kuendesha Ofisi Kuu na mahitaji yote ya Ofisi na hiyo itaonyesha hofu ya Mungu na Uaminifu ndani ya Mchungaji husika.

FUNGU LA PILI

Sifa ya Kuunda Kanisa la Mahali.

World Revival Ministries, Tanzania na World Revival Church of Tanzania kwa pamoja tunaamini yafuatayo katika kuunda sifa za KANISA LA MAHALI hapa Tanzania

- a) Awepo Mchungaji Kiongozi mwenye mwito aliyethibitishwa na Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa kwa kufuata Kifungu cha 11(2) cha Katiba ya World Revival Ministries, Tanzania ya mwaka 2002.
- b) Kanisa la Mahali lazima liwe na Waamini si chini ya **250** na kuendelea na lenye kusimamia Makusanyiko mengine ya Waamini yatakayoitwa **KANISA LA PARISHI**.
- c) Ardhi ya Kanisa la Mahali liwe limenunuliwa kwa kutumia Jina na Usajili wa World Revival Ministries, Tanzania na World Revival Church.
- d) Mchungaji Kiongozi wa WORLD REVIVAL CHURCH atateua Wachungaji Wasaidizi, Wazee wa Kanisa, Mashemasi na Viongozi wengine baada ya kuteuliwa na Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji wa World Revival Ministries, Tanzania kwa kufuata Kifungu cha 11(2) cha Katiba yake.
- e) Wachungaji Wasaidizi, Wazee wa Kanisa, Mashemasi na Mhasibu wa Kanisa baada ya kuteuliwa na Mchungaji Kiongozi ndani ya World Revival Church kabla ya kutumika ndani ya Kanisa la Mahali lazima **waidhinishwe** kwanza na **BARAZA LA WAAMINI** au WASHIRIKI kwa kufuata Kanuni ya World Revival Ministries, Tanzania ya mwaka 2009 **Kifungu cha Kumi na Tisa (19)**.
- f) Kanisa la Mahali lililokidhi vigezo kuanzia (a) hadi (e) litawajibika kiutendaji kila siku kwenye Ofisi ya Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa sawasawa na Kifungu cha 11(2) cha Katiba ya World Revival Ministries, Tanzania ya mwaka 2002.
- g) Makanisa yanaweza kuwa chini ya Kanisa la Mahali lenye vigezo au sifa mpaka hapo makanisa hayo yatakapopata sifa au vigezo vya kuwa KANISA LA MAHALI ndani ya World Revival Ministries, Tanzania na World Revival Church na makanisa hayo yatakuwa matawi ya Kanisa la Mahali lenye sifa au Makanisa hayo yataitwa **PARISH**.
- h) Hata hivyo **World Revival Church of Tanzania** ni KANISA LA MAHALI kutoka nchi nyingine hapa duniani yenye Makao Makuu Sekei, Jiji la Arusha- Tanzania.
- i) World Revival Ministries, Tanzania inaelekeza kila Mchungaji Kiongozi, kila Muumini na kila Kiongozi kufuata Katiba (**2002**), Maelezo ya Imani(**2009**), Kanuni(**2009**) na Maelekezo ya Mtumishi(**2002**) ya World Revival Ministries, Tanzania.

FUNGU LA TATU

1.0.Huduma Kuu Tatu (3)

World Revival Ministries, Tanzania katika kutimiza AGIZO KUU LA YESU KRISTO hapa duniani sawasawa na (Matayo 28:18-20 na Marko 16:15-20) inaendelea na itaendelea kujikita katika huduma mbalimbali hapa duniani.

1.1. WORLD REVIVAL CHURCH

World Revival Ministries, Tanzania katika kuhubiri Injili ya Yesu Kristo watu wengi wanamwamini YESU KRISTO kuwa Bwana na Mwokozi na kufanyika Mwili wa Yesu Kristo au Kanisa la Yesu Kristo au Nyumba ya Mungu sawasawa na Yohana 1:12-14, Matendo ya Mitume 2: 1-45 na Matayo 28:18-20, Matendo ya Mitume 1:8, Warumi 12:4-5. 1 Wakorintho 4:1-16, 12:13, 27-28, 14:12 na Waefeso 2:19-22 Waamini hao ambao wamemwamini Yesu Kristo kuwa Bwana na Mwokozi ndani ya World Revival Ministries, Tanzania wataitwa **THE WORLD REVIVAL CHURCH** na itatekezwa sawasawa na Kifungu cha 7(1), 10(x) na 11(2) na 18(b)iv cha Katiba ya WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA ya mwaka wa Bwana Yesu Kristo (2002).



- a) World Revival Church na Uongozi wake kuanzia ngazi ya Kanisa la Mahali mpaka Taifa watafuata Katiba(2002), Maelezo ya Imani(2009), Kanuni(2009) na Maelekezo ya Mtumishi(2002) katika kuongoza Waamini hao ndani ya World Revival Church.
- b) Kamati ya Utendaji na Bodi ya Wadhamini wa World Revival Ministries, Tanzania ni Viongozi wa World Revival Church kitaifa na wataongoza Waamini wote ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
- c) Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa au Mwangalizi wa World Revival Church ataendelea kuongoza kitaifa WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA na WORLD REVIVAL CHURCH katika kuendesha shughuli zote za kila siku na ndiye mwenye mamlaka ya kiutendaji na kihuduma na kuruhusu Mchungaji Kiongozi yeyote kutumika ndani ya timu yetu ya WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA katika

kuchunga Waamini kwa kufuata Katiba ya World Revival Ministries, **Tanzania kifungu cha 11(2) tu.**

- d) Mchungaji mpya atajaza fomu ya Utumishi na kupewa barua ya kumtambulisha kwenye Ofisi za Serikali ili asiweze kusumbuliwa katika kuleta watu wengi kwa YESU KRISTO na barua hiyo itatolewa na Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa au Mwangalizi Mkuu wa nchi na kwa kigezo hicho ni marufuku mtumishi yeyote kutumia Jina na Nembo ya WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA na WORLD REVIVAL CHURCH bila kibali cha Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa kwa kufuata Kifungu cha 11(2) cha Katiba ya WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA na Usajili wake.
- e) World Revival Ministries, Tanzania kwenye ngazi ya kanisa la mahali litaongozwa na Mchungaji Kiongozi atakayethibitishwa na Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa na pia ataweza kuondolewa na Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa baada ya kujadiliwa Mchungaji Kiongozi huyo kwenye Kamati ya Utendaji na Baraza Kuu la Kanisa, **Mchungaji Kiongozi ni Mtumishi wa Mungu** ndani ya **Ofisi ya Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa** ndani ya Ofisi kuu katika kusimamia Kanisa na atawajibika kwa kila tendo kwa Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa kwa shughuli za kila siku.
- f) World Revival Church kwenye ngazi ya Mkoa na Wilaya itaongozwa na Askofu wa Mkoa au Wilaya ambao watateuliwa na Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa ili kusimamia Makanisa ya Mahali ndani ya Mkoa na Wilaya na viongozi wote hao watawajibika kwa Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa kiutendaji kwa shughuli za kila siku ndani ya Ofisi ya Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa, Viongozi hao pia ndani ya mkoa na wilaya wataondolewa na Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa bila kushirikisha Kamati ya Utendaji taifa na Baraza Kuu la Kanisa baada ya kuona Utendaji wao usioridhisha ndani ya mkoa na wilaya.
- g) World Revival Church kwenye ngazi ya taifa litaongozwa na Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa ambaye atachaguliwa/ kuteuliwa/ kuthibitishwa na **Bodi ya Wakurugenzi na Wadhamini**, **Wachungaji Viongozi** waliowekewa mikono(Ordained Pastors) na **Waanzilishi** wa World Revival Ministries, Tanzania na World Revival Church na pia ataondolewa kazini na Bodi ya Wadhamini na Wakurugenzi wa WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA.

FUNGU LA NNE

1.2. Maelezo ya Msingi ya Mchungaji Kiongozi

World Revival Ministries, Tanzania inatoa maelekezo ya msingi kwa kila Mchungaji Kiongozi au yeyote mwenye nia njema ya kuanzisha au kupanda Kanisa au kuchunga Waamini ndani ya WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA hapa Tanzania na

ambaye anataka kukusanya waamini sehemu moja atalazimika kufuata kwa uaminifu, upole, weledi, unyenyekevu mbele za Mungu na Wanadamu katika kusimamia yafuatayo:-

1.Kwa kufuata Katiba (2002), Maelezo ya Imani(2009), Kanuni(2009) na Maelekezo ya Mtumishi(2002) za WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA inatambua kuwa WORLD REVIVAL CHURCH ni Kanisa la Kiroho, Kanisa la Kipentekoste sawasawa (Yohana 1:12-14, Matayo 28:18-20, Marko 16:15-20 na Matendo ya Mitume 2:1-45) ambalo limethibitishwa kuwepo kwa Waamini kupitia Agizo Kuu la Yesu Kristo Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa baada ya kujiridhisha na kuruhusu Mchungaji Kiongozi kutumika sawasawa na Katiba ya WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA kifungu cha 11(2). Mchungaji Kiongozi wa Kanisa atapokea nyaraka zifuatazo kutoka kwa Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa

- a) Barua ya kumtambulisha Mchungaji Kiongozi kwenye serikali
- b) Cheti kivuli cha WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA
- c) Katiba ya World Revival Ministries, Tanzania(2002)
- d) Maelezo ya Imani ya World Revival Ministries, Tanzania(2009)
- e) Kanuni za World Revival Ministries, Tanzania(2009)
- f) Maelekezo ya Mtumishi ya World Revival Ministries, Tanzania(2002)
- g) Neno la Mungu(THE BIBLE)
- h) Tenzi za Rohoni(Nyimbo za Tenzi)

2.World Revival Ministries, Tanzania inatambua huduma ya Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa kama Mtendaji Mkuu ndani ya Kanisa la Mahali na mwenye mamlaka ya kuteua Mchungaji Kiongozi wa Kanisa husika na pia ametoa mamlaka kwa Mchungaji Kiongozi kuteua wasaidizi wake kwenye Kanisa. Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa atasimamia makanisa ya mahali yote pamoja na Wachungaji Viongozi katika kusimamia Waamini ndani ya WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA kwa kufuata Katiba ya World Revival Ministries, Tanzania kifungu cha 11(2) ya mwaka 2002.

3.Mchungaji Kiongozi au Kiongozi yeyote wa WORLD REVIVAL CHURCH ndani ya WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA atalazimika kuwa na IMANI YA KIPENTEKOSTE sawasawa na Maelezo ya Imani ya mwaka 2009 ya WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA na Imani ya World Revival Church sawasawa na Kanuni ya WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA ya mwaka 2009 na kufuata Neno la Mungu (Yohana 1:12-14, Matendo ya Mitume 2:1-45, Matayo 28:18-20 na Waefeso 4:1-18).

4.Mchungaji Kiongozi au Mtumishi yeyote wa WORLD REVIVAL CHURCH ndani ya WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA atalazimika kutumia NENO LA MUNGU (THE BIBLE) na MAOMBI NA MAOMBEZI katika huduma zake zote ili kusaidia Waamini na Wasio Waamini.

5. **WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA** na **WORLD REVIVAL CHURCH** zitaendeshwa kwa nguvu ya **ROHO MTAKATIFU** kupitia **MTUMISHI WA MUNGU WA KIUME** na **MTUMISHI WA MUNGU WA KIKE** kwenye Mekanisa ya Mahali Nchini Tanzania.

6. Mchungaji Kiongozi ndani ya **WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA** atakuwa na mamlaka ya kuteua Wachungaji wasaidizi, Wazee wa Kanisa, Wachungaji wa Idara za Kanisa, Mashemasi wa Kanisa ambao wote watawajibika kiutendaji kwa Mchungaji Kiongozi kwa kufuata Kanuni za World Revival Ministries, Tanzania ya mwaka 2009 na baada ya kuwateua Mchungaji Kiongozi ataitisha kikao cha Baraza la Waamini au Washiriki wa Kanisa ili majina hayo yaidhinishwe rasmi sawasawa na kifungu cha kumi na tisa(19) cha Kanuni za **WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA** ya mwaka 2009.

7. Waamini wote ndani ya World Revival Ministries, Tanzania na World Revival Church wataongozwa na Neno la Mungu (The Bible), Katiba (2002), Maelezo ya Imani(2009), Kanuni(2009) Maelekezo ya Mtumishi(2002) pamoja na Tenzi za Rohoni.

8. **WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA** NA **WORLD REVIVAL CHURCH** zitaendelea kushirikiana na watumishi wengine kutoka Mekanisa ya Kipentekoste Kiimani hapa Tanzania na nchi nyingine duniani katika kuleta watu wengi kwa **YESU KRISTO** sawasawa na Matayo 28:18-20 na Marko 16:15-20.

9. Mchungaji Kiongozi aliyewekewa mikono ataweza kuchaguliwa kuwa Askofu wa Mkoa au Wilaya na kuwa na haki ya kupata leseni ya kufungisha ndoa.

10. Wachungaji Viongozi wote wa Kanisa walioidhinishwa na kupata barua ya Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa sawasawa na Kifungu cha 11(2) cha Katiba ya **WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA** wataendesha huduma zao bila kuingiliwa **KIFEDHA** na **UONGOZI** isipokuwa mambo yafuatayo yataingilia **UHURU** wao wa kihuduma ili kukidhi matakwa ya kisheria na Katiba ya World Revival Ministries, Tanzania ya mwaka 2002.

(i) **Kutoa taarifa ya mapato na matumizi ya Kanisa analosimamia kila mwaka wa fedha kwenye Ofisi ya Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa wa WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA na WORLD REVIVAL CHURCH.**

(ii) **Kutoa taarifa ya Kanisa/Huduma mara kwa mara kupitia vikao au njia nyingine wezeshi kwa ASKOFU MKUU na MWENYEKITI MTENDAJI TAIFA.**

(iii) **Kila Mchungaji Kiongozi wa World Revival Ministries, Tanzania na World Revival Church analazimika kutoa FUNGU LA KUMI kwa ASKOFU MKUU na MWENYEKITI MTENDAJI TAIFA ambaye ni Msimamizi Mkuu ndani ya Kanisa ambaye anasimamia Waamini wote na Wachungaji Viongozi wote ndani ya WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA na WORLD REVIVAL CHURCH. Hata hivyo Ofisi ya Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa**

itapokea Fungu la Kumi kutoka kila Kanisa kwa sadaka zote zinazotolewa na Waamini kwa ajili ya kuendesha Ofisi Kuu kwa ajili ya mahitaji yafuatayo:-

- a) Kusafirisha Mtumishi aliyetumwa na Ofisi ya Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa kwa shughuli za Kitaifa.
- b) Tukio lolote la serikali linalohitaji fedha za Kanisa.
- c) Safari za Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa na Wasaidizi wake kutembelea Mkanisa ya Mahali.
- d) Sadaka ya Fungu la Kumi(10%) itatumika kuandalia vikao vya kitaifa vinavyoandaliwa na Ofisi ya Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa.
- e) Kusaidia mambo yote ya Kiofisi ya Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa pamoja na mambo mengine.

11.Mchungaji Kiongozi anayetoa Fungu la Kumi kutoka sadaka ya Kanisa na mapato yake mwenyewe kwa Uaminifu, Uadilifu, Unyenyekevu ataheshimika ndani ya WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA na WORLD REVIVAL CHURCH na pia kwenye Ofisi ya Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa au **OFISI KUU** na ni **AIBU kubwa Mchungaji Kiongozi** ambaye ni Kiongozi ndani ya **OFISI YA ASKOFU MKUU na MWENYEKITI MTENDAJI TAIFA** ambaye ameaminiwa sana na Kanisa anayevunja **NENO LA MUNGU** kwa makusudi **anajiondolea** Heshima ya Utumishi ndani ya WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA hata **kutoaminika** kabisa kwa mambo makubwa kwa kuiba zaka kwa kudanganya **ROHO MTAKATIFU** kwa **kutotenda** sawasawa na **NENO LA MUNGU** katika kuwaongoza Waamini au Kanisa na pia **Suala hili la Utoaji kwa uaminifu, upole, unyenyekevu na uadilifu** linahusu Waamini wote ndani ya Kanisa la Mahali kwa ajili ya Utukufu wa Mungu.

12.Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa atawekea mikono Mchungaji Kiongozi au Askofu wa mkoa au wilaya ndani ya WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA na WORLD REVIVAL CHURCH kati ya mwaka 1 hadi 10 tangu alipoidhinishwa na Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa na kama **MTUMISHI** huyo hana sifa ya kuwekewa mikono basi zoezi hilo halitafanyika. Kwa Mchungaji Kiongozi au Askofu wa Mkoa au Wilaya atakidhi vigezo basi hatua tatu zitafuatwa kama ifuatavyo:-

- a) **Kanisa la Mahali chini ya Mchungaji Kiongozi na Baraza la wazee wataunda Kamati ya Sherehe kwa tarehe itakayotajwa na Ofisi ya ASKOFU MKUU na MWENYEKITI MTENDAJI TAIFA.**
- b) **Ofisi ya Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa itaanda ORDINATION CERTIFICATE, KATIBA, MAELEZO YA IMANI, KANUNI, MAELEKEZO YA MTUMISHI, BIBLIA NA TENZI ZA ROHONI** kwa ajili ya kumpatia Mchungaji Kiongozi anayetarajiwa kuwekewa mikono.
- c) **ORDINATION CERTIFIACATE** ikipokelewa mbele ya Kanisa (Waamini) kwa kuliongoza Kanisa mpaka Yesu Kristo atakaporudi kulichukua hapa duniani bali asivunje **Neno la Mungu, Katiba (2002), Maelezo ya Imani (2009), Kanuni(2009) na Maelekezo ya Mtumishi (2002).**

13. World Revival Church ndani ya World Revival Ministries, Tanzania katika kusimamia Waamini waliompokea YESU KRISTO kuwa Bwana na Mwokozi wao sawasawa na Yohana 1:12-14, Matendo ya Mitume 2:1-45 wataendelea kutumia **NEMBO** ya Kanisa (Waamini) ndani ya WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA na kuendelea kusifu Mungu, kuabudu Mungu, kufanya Maombi na Maombezi, kufanya mahusiano na Mungu wao kupitia kusoma NENO LA MUNGU na kazi yao kubwa ikiwa ni kuendelea kuleta watu wengi kwa YESU KRISTO sawasawa na Matayo 28:18-20 na Marko 16:15-20 hapa duniani.

1.2. WORLD REVIVAL COLLEGE OF THEOLOGY.

- (i) Huduma hii ndani ya WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA itaendelea kutekelezwa kwa kufuata kifungu cha 10(ii) cha Katiba ya World Revival Ministries, Tanzania ya mwaka 2002 kwa ajili ya kuhimiza Wachungaji Viongozi, Mitume, Walimu wa Neno, Wainjilisti, Manabii na Wakristo wote wenye nia ya kusoma theolojia kutoka Mkanisa ya Kipentekoste kwenye vyuo ambavyo vinatambuliwa na Mkanisa ya Kipentekoste hapa duniani.
- (ii) Huduma hii itaendelea kuhimiza watumishi wa Mungu kupata ujuzi wa KIROHO kwahiyu WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA kupitia WORLD REVIVAL COLLEGE OF THEOLOGY itawezesha kushirikiana na vyuo vya theolojia katika kusaidia Watumishi wote wenye miito na vipawa ndani ya Mkanisa ya Kipentekoste hapa Tanzania.

1.3. WORLD REVIVAL HUMANITARIAN FUND

- (i) Huduma hii ndani ya WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA inakusudia kusaidia makundi yasiyojiweza ndani ya jamii zetu sawasawa na Yakobo 1:25-27, Isaya 58:5-9, na Isaya 1:15-20 na pia kupitia vifungu vya 7(ii)8, 10(iv), 10(xii) vya Katiba ya WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA ya mwaka 2002.
- (ii) Kila Mchungaji Kiongozi ndani ya WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA na WORLD REVIVAL CHURCH asimamie MFUKO huu kwa kuweka utaratibu maalum na sadaka maalum ya kusaidia wasiojiweza ndani ya jamii inayotuzunguka kwa kusimamia NENO LA MUNGU TAKATIFU
- (iii) MFUKO huo utasimamiwa na Mashemasi wa Kanisa la Mahali na Mchungaji Kiongozi na Mashemasi wa Kanisa la Mahali wanaunda Kamati ya Utendaji wa Mfuko huo na Mchungaji Kiongozi ndiye MWENYEKITI wa Mfuko huo ndani ya WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA na WORLD REVIVAL CHURCH katika kuhudumia watoto Yatima na Makundi mengine yasiyojiweza kabisa na pia angalizo kwa Kamati ya Mfuko hakikisha sheria za nchi ya Tanzania zinafuatwa katika kulinda watoto na makundi mengine.
- (iv) NOTE: Huduma Kuu Tatu(3) ni sehemu ya nyingi zinazohitajika kufanyika kwa kufuata Malengo ya Katiba ya WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA.

FUNGU LA TANO

Kanisa la Parishu

World Revival Ministries, Tanzania itaendelea kukusanya Waamini wasiozidi **250** sehemu moja kwa ajili ya Kusifu Mungu, Kuabudu Mungu, Kuomba Mungu, Kusoma Neno, Maombi na Maombezi na kutafuta Mahusiano na Mungu kila Wakati na pia kuendelea kuleta Watu wengi kwa Yesu Kristo. World Revival Ministries, Tanzania litaanzisha mikusanyiko ya Waamini itayoitwa **Kanisa la Parishu** ambayo yatafuata taratibu zifuatazo:-

- (i) Kanisa la Mahali litajengwa na Parishu mbalimbali zenye Idadi ya Waamini kuanzia **0** hadi **250** ndani ya WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA,
- (ii) Kanisa la Mahali lazima liwe na Mkusanyiko wa Waamini usiopungua **250** na kuendelea, Mchungaji Kiongozi aliyethibitishwa na Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa sawasawa na Kifungu cha 11(2) cha World Revival Ministries, Tanzania ya mwaka 2002 ataongoza Waamini hao **250** na kuendelea.
- (iii) Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la Mahali huyo kwa mamlaka aliyonayo atateua Wachungaji Wasaidizi, Wazee wa Kanisa, Mashemasi, na viongozi wengine ndani ya Kanisa la Mahali na kabla ya Watumishi hao kufanya kazi ya Kanisa la Mahali majina yao yataidhinishwa na **BARAZA LA WAAMINI** au WASHIRIKI sawasawa na Kifungu cha Kumi na Tisa (**19**) cha Kanuni ya WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA ya mwaka 2009.
- (iv) **Mchungaji wa Kanisa la Parishu** atateuliwa na Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa sawasawa na Kifungu cha 11(2) cha Katiba ya WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA ya mwaka 2002, Hata hivyo Wazee wa Kanisa na Mashemasi wataidhinishwa na Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la Mahali na Baraza la Wazee wa Kanisa la Mahali.
- (v) Wazee wa Kanisa wa Parishu na Mashemasi wa Kanisa la Parishu baada ya kuteuliwa na Mchungaji Kiongozi na Wazee wa Kanisa wa Kanisa la Mahali kabla ya kufanya kazi hiyo wataidhinishwa na Baraza la Waamini au Wahiriki wa Kanisa la Mahali tu na **si** Kanisa la Parishu.
- (vi) Mchungaji wa Parishu pamoja na viongozi wengine wa Parishu kwa panoja watawajibika kiutendaji kwa shughuli za kila siku kwa Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la Mahali.
- (vii) Kanisa la Parishu litafuata maelekezo yote yanayofuatwa na Kanisa la Mahali kwa kuwa **Parishu iko chini ya Kanisa la Mahali** kwa kufuata Katiba(2002), Maelezo ya Imani(2009), Kanuni(2009) na Maelekezo ya Mtumishi(2002).

FUNGU LA SITA

Kibali cha Mtumishi Mbele ya Serikali.

- (i) World Revival Ministries, Tanzania ni Huduma ya Kiroho katika kufikia watu mbalimbali hapa duniani sawasawa na Matayo 28:18-20 na Marko 16: 15-20 ambalo ni Agizo Kuu la Yesu Kristo aliloliacha kwetu kabla ya kutuacha kwenda Mbinguni.
- (ii) World Revival Ministries, Tanzania inatambua uwepo wa serikali na mamlaka zake kupitia Katiba ya Nchi na Sheria zake kwa ajili ya kusimamia watu wake na hao watu pia tunawafikia na Injili ya YESU KRISTO hapa duniani .
- (iii) World Revival Ministries, Tanzania kwa kuwa na lengo la kufikia watu na Injili ya YESU KRISTO itaendelea kufuata Katiba na Sheria za Nchi pia ili kulinda UMISHENI wake hapa duniani.
- (iv) Yesu Kristo alizikuta serikali za dunia na alifanya **MAPENZI YA MUNGU** pekee yake na alimaliza kazi yake ya kumkomboa mwanadamu na dhambi zake na alimkomboa mwanadamu mbali na nguvu za Shetani na Malaika zake, **kila Mchungaji Kiongozi aongoze Kanisa la Yesu kwa kufanya Mapenzi ya Mungu pekee yake.**
- (v) World Revival Ministries, Tanzania kwa kuwa inashirikiana na serikali ambazo zinalinda watu wake kwa kufuata Katiba na Sheria za nchi husika Basi World Revival Ministries, Tanzania inalazimika kukusanya taarifa za Mtumishi ambaye atahudumia watu ambao wanamilikiwa na kulindwa na serikali za nchi na pia Mtumishi wa Mungu atapewa utambulisho wa barua mbele ya serikali ili asisumbuliwe na mtu yeyote na sehemu yoyote kwa kuwa World Revival Ministries, Tanzania imefuata sheria za nchi kwa kuwa na kibali cha nchi ya Tanzania kwa ajili ya kueneza Injili ya YESU KRISTO.
- (vi) MTUMISHI WA MUNGU ndani ya WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA lazima aidhinishwe na Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa kwa kupewa kibali cha MTUMISHI mbele ya serikali baada ya kupata taarifa zake binafsi na Huduma zake za Kiroho ambazo Mungu amempatia kufanya hapa duniani.
- (vii) WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA inaelekezo kila Mtumishi ambaye anatumia leseni yetu afuate Katiba(2002), Maelezo ya Imani(2009), Kanuni (2009) na Maelekezo ya Mtumishi (2002) ili kuendelea kutii Katiba na Sheria za Nchi ya Tanzania na World Revival Ministries, Tanzania kutoingia mgogoro na Serikali kwa Mtumishi kushindwa kufuata Mwongozo wa WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA ulioidhinishwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

©WRMT/MAELEKEZO YA MTUMISHI-2002

TAARIFA ZA MTUMISHI

Jina la Mtumishi.....

Namba ya Simu.....

Baruapepe.....

Anuani.....

Jinsia.....

Tarehe ya Kuzaliwa.....

Mkoa na Wilaya ulikozaliwa.....

Kata na Kijiji au Mtaa.....

Kitongoji.....

Unaishi kwa sasa Mkoa na Wilaya.....

Kata ya.....Kijiji/Mtaa.....

Kitongoji.....

Namba ya Nida.....

Chagua huduma yako kati ya hizi hapa kwa kufuta isiyohitajika **MCHUNGAJI, MTUME, MWINJILISTI, MWALIMU WA NENO, NABII na MWIMBAJI**

.....
.....

Kabla ya kujiunga na **WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA** umetumika na huduma zipi, zitaje

.....
.....

Je uko tayari kufuata Katiba (2002), Maelezo ya Imani(2009), Kanuni(2009) na Maelekezo ya Mtumishi (2002) ya **WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA**.

Ndiyo /Hapana.....

Kama ni Hapana toa sababu.....

KIAPO CHA HUDUMA MTUMISHI.

Mimi **nimesoma, nimeelewa, nakubali na niko tayari** kufuata Katiba(2002), Maelezo ya Imani(2009), Kanuni(2009) na Maelekezo ya Mtumishi(2002) ya **WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA** na pia nimekubali IMANI na MADHUMUNI ya WORLD REVIVAL CHURCH na kwa kuwa nimekubali nitasimamia, nitalinda na kuendeleza kazi ya YESU KRISTO kwa weledi, uaminifu na uadilifu

Mungu naomba unisaidie.

Jina la Mtumishi.....

Sahihi ya Mtumishi.....

Dole Gumba la Mtumishi.....

KWA MATUMIZI YA OFISI TU

Mimi **Apostle Dr. Bukuri A Masago** namthibitisha Mchungaji / Mtume.....kuwa sehemu ya Timu ya **Watumishi wa Mungu** ndani ya WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA na WORLD REVIVAL CHURCH na kuwa atasimamia Katiba (2002), Maelezo ya Imani (2009), Kanuni(2009) na Maelekezo ya Mtumishi(2002) ya WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA na pia atasimamia IMANI na MADHUMUNI ya World Revival Church.

.....

Apostle Dr.Bukuri A Masago

Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa

SHAHIDI WA KISHERIA.

Jina la Wakili.....

Sahihi ya Wakili.....

Mhuri wa Wakili

WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA (W.R.M.T)

“The Outreach Ministry for Gospel of Jesus Christ on the Earth”



P.O.BOX 6712 MOSHI-TANZANIA

Email: worldrevivalministries@yahoo.com

Phone: +255 786 198623, +255790198623

Tarehe.....

REF.No.WRMT/SA/17453/VOL1/.....

MKUU WA WILAYA

WILAYAYA.....

S.L.P.....

.....,TANZANIA

Ndugu,

YAH: UTAMBULISHO WA MTUME NA MCHUNGAJI.....

1.Rejea kichwa tajwa hapo juu,

2.World Revival Ministries,Tanzania ni taasisi ya Kidini yenye Usajili No. **SA.17453** kwa ajili ya kueneza Injili ya YESU KRISTO hapa duniani sawasawa na Matayo 28:18-20 na Marko 16:15-20.

3.Mtajwa hapo juu na **picha yake** iliyoambatanisha ni miongoni mwa Wachungaji na Mitume ndani yaWORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA na ataongoza **Waamini** (THE WORLD REVIVAL CHURCH) katika Mtaa/ Kijiji.....Kata yaWilaya ya.....Mkoa wa.....

4.Kwahiyo Ofisi ya **WORLD REVIVAL MINISTRIES, TANZANIA** inamtambulisha kwenye **Uongozi wa Serikali** na mmpatie ushirikiano ili afanye majukumu yake kulingana na Katiba ya World Revival Ministries, Tanzania ya mwaka 2002.

5.Wenu katika kazi ya kujenga Ufalme wa Mungu katika **YESU KRISTO** na kujenga Taifa la Tanzania.

.....

Apostle Dr. Bukuri A Masago

Askofu Mkuu na Mwenyekiti Mtendaji Taifa

World Revival Ministries, Tanzania